NSSF EMPLOYEES SACCOS
Tunawezesha Kufikia Ndoto Zako

**CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO CHA WAFANYAKAZI WA NSSF**

**(NSSF EMPLOYEES SACCOS LTD)**

**S.L.P 19910, DAR ES SALAAM.**

**DSR. 2056**

# MKATABA WA MKOPO

**Baina ya**

**NSSF SACCOS LIMITED**

(Ambaye ni MKOPESHAJI)

**NA**

**Ndugu: ..............................................................................................**

**Wa S.L.P......................................... Simu: .........................................**

(Ambaye ni MKOPAJI)

**Mkataba huu umetayarishwa na:**

**NSSF EMPLOYEES SACCOS LIMITED**

**MKATABA WA MIKOPO**

Mkataba huu umefanyika leo siku ya tarehe ……… ya mwezi……….**.**mwaka 20…**…….**

Baina ya Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Wafanyakazi wa NSSF chenye namba ya usajili **DSR 2056** kilichoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013, (na Kanuni zake) na anwani yake ni S.L.P 19910, DAR ES SALAAM (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama **MKOPESHAJI**) kwa upande mmoja.

Ndugu ………………………………………………………………………………**.**ambaye ni Mwanachama wa Chama mwenye namba ………….. katika Daftari la Wanachama, wa S.L.P ………………………………………**.** na mwenye namba ya simu……………………………….(ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama **MKOPAJI)** na neno **"Mkopaji"** linaweza kujumuisha Warithi wa mali za Mkopaji, Wamiliki, Wasimamizi au Wadhamini wake, kadri itakavyohitajika), kwa upande mwingine.

**KWA KUWA**:

(i) **MKOPESHAJI** baada ya kuzingatia maombi yaliyowasilishwa na **MKOPAJI** amekubali kumpatia huduma ya mkopo **MKOPAJI** kwa mujibu wa Masharti na Sera ya Mikopo ya Chama.

(ii) **MKOPAJI** ameomba kwa hiari yake kupatiwa huduma ya mkopo kutoka kwa **MKOPESHAJI**.

(iii) **MKOPESHAJI** ambaye ni Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo kilichoanzishwa kwa mujibu wa Sheria.

(iv) **MKOPESHAJI** ambaye amekubali kumpatia huduma ya mkopo MKOPAJI.

(v) **MKOPAJI** ni Mwanachama hai wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Wafanyakazi wa NSSF.

(vi) **MKOPAJI** amekubali kupewa huduma ya mkopo kutoka kwa **MKOPESHAJI**.

**KWA HIYO BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA KWAMBA:-**

1. Baada ya kutiwa saini kwa mkataba huu, Mkopeshaji atampatia Mkopaji mkopo wenye thamani ya fedha za kitanzania Tshs………… yaani ……….... (Taja kiasi kwa maneno) na Mkopaji anakiri kupokea kiasi kilichotajwa.
2. Mkopaji anaahidi kuwa atarejesha mkopo aliouchukua wenye riba ya Tshs. ……………….yaani ……………..(Taja kiasi kwa maneno) kwa kipindi cha miezi ……………( ) kwa maana hii, Mkopaji atarejesha Mkopo huokikamilifu pamoja na riba yote kabla ya au ifikapo terehe ……………..mwezi……………..mwaka 20……
3. Mkopaji atafanya marejesho kila mwezi kulingana na jedwali la marejesho lililoambatishwa kwenye Mkataba huu.
4. Mkopaji akishindwa kufanya marejesho ya kila mwezi kikamilifu (mkopo msingi na riba) kwa mujibu wa jedwali lililoambatishwa, atapata adhabu ya asilimia ….. kwa kila mwezi husika.
5. Mkopaji ameweka mali zilizotajwa hapa chini kama dhamana ya mkopo ambazo pamoja na ; hisa za hiari, akiba na dhamana za wadhamini zitatumika kulipa deni iwapo Mkopaji atashindwa kulipa deni hilo kwa wakati

   **(i) Hisa za hiari zenye thamani ya Tshs. ……… (kwa maneno) Shilingi……………………………………**

**(ii) Akiba zenye thamani ya Tshs. ……… (Taja kiasi kwa maneno) Shilingi……………………………………………………**

**(iii) Mali ya Mkopaji iliyopo (a)…………….. (b)……………………(taja aina ya mali na eneo/mahali dhamana ilipo).**

**(iv) Mali za Wadhamini/Mdhamini: (1)………….zenye thamani ya Tshs……… (Taja kiasi kwa maneno) Shilingi ……………… (taja aina ya mali, thamani yake na eneo/mahali dhamana zilipo)……………………. (2)………….zenye thamani ya Tshs……… (Taja kiasi kwa maneno) Shilingi ……………… (taja aina ya mali, thamani yake na eneo/mahali dhamana zilipo) ………………………………..**

6. Kwa mujibu wa Mkataba huu, mkopaji, mrithi/warithi wa mkopaji au Mdhamini/Wadhamini wa mkopaji hawataruhusiwa kuhamisha umiliki, kuuza, kupunguza au kutumia kama dhamana, mali iliyowekwa dhamana hadi deni lote (litakalohusisha; mkopo msingi, riba pamoja na adhabu kama itakuwepo) litakapokuwa limelipwa.
7. Mkopaji akishindwa kulipa deni lote (litakalohusisha; mkopo msingi, riba pamoja na adhabu kama itakuwepo) au kimoja wapo katika muda uliopangwa, Mkopeshaji atakuwa na haki ya kuchukua hatua za kisheria kukomboa deni lake ikiwa ni pamoja na kutwaa na kumiliki dhamana iliyowekwa au kuuza dhamana hiyo ili kulipa deni bila kulazimika kuomba mamlaka ya kisheria ya kufanya hivyo, baada ya kumtaarifu Mkopaji kwa Maandishi.
8. Iwapo Mkopaji atashindwa kulipa deni lote na riba au kimojawapo na Mkopeshaji akaamua kuchukua hatua za kisheria kama ilivyokubaliwa katika kipengele cha "5" hapo juu, ikiwa ni pamoja na kutwaa mali ya dhamana, kuuza au kufungua shauri ili kudai au kufidia deni na gharama zote za kutekeleza hatua hizo zitalipwa na Mkopaji.
9. Kwa mujibu wa Mkataba huu, Mdhamini/Wadhamini watawajibika wakati wowote kumhimiza Mkopaji kulipa deni lake na kwamba ikitokea mkopaji

ameshindwa kulipa deni lake hatua za kisheria zilizotajwa katika sharti la tano na sita (5 na 6) hapo juu zitachukuliwa dhidi ya Mdhamini au Wadhamini wa Mkopaji.

10. Mkopaji anakubali taarifa zilizotolewa ndani ya Mkataba huu zitutmike katika usimamizi wa mikopo.
11. Mkataba huu, hautaathiri masharti mengine ya lazima kuhusu mikopo yaliyowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha pamoja na Kanuni zake, Masharti ya Chama pamoja na Sera ya Mikopo.
12. Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha pamoja na Kanuni zake zitatumika kutatua suala au mgogoro wowote kuhusu Mkataba huu.
13. Mkopaji anaridhia taarifa za mikopo au mkopo wake kuwasilishwa kwa taasisi zinazochakata taarifa za Wakopaji Tanzania (Credit Bureau) muda wowote pasipo kutaarifiwa.
14. Fomu ya mkopo na fomu nyingine zitakazosainiwa na mkopaji zitakuwa sehemu ya mkataba huu.
15. Tarehe aliyopata mkopo…………………........
16. Tarehe ya kuanza kulipa ………………………..
17. Tarehe ya kumaliza kulipa ………………………
18. Kiwango cha Riba …………………………….% (kwa mwezi/mkupuo)

**KWA KUZINGATIA USHUHUDA ULIOTOLEWA HAPO JUU, MKATABA HUU UMESAINIWA NA WAHUSIKA SIKU, TAREHE, MWEZI NA MWAKA KAMA IFUATAVYO.**

Mkataba huu umefikiwa na kushuhududiwa leo tarehe…………. mwezi………….. mwaka…………………… kama unavyoonesha hapa chini kati ya MKOPESHAJI na MKOPAJI

Umetiwa muhuri na NSSF EMPLOYEES SACCOS Limited na umepokelewa mbele yetu tarehe ………………. mwezi …………………… mwaka …………………….

**UMESAINIWA na KUPOKELEWA NA:**

……………………………………………………… ambaye
anaelewa lugha iliyotumika katika uandaaji wa Mkataba
huu leo tarehe …………………mwezi………mwaka 20……

…………………………….
Saini ya Mkopaji

**UMESAINIWA na KUTOLEWA NA:**

……………………………………………………… ambaye
anaelewa lugha iliyotumika katika uandaaji wa Mkataba
huu leo tarehe …………………mwezi………mwaka 20……

…………………………….
Saini na Muhuri
wa Mkopeshaji

(Tamko hili ni lazima litolewe mbele ya waliotajwa hapo chini)

MBELE YANGU KAMISHINA WA VIAPO/WAKILI/HAKIMU/MDHAMINI WA MKOPO

JINA: ………………………………………………………………………

SAINI: ……………………………………

ANUANI/SIMU: ………………………………………………………

WADHIFA: …………………………………